## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MEI, 2025 NA MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2025.

**Dondoo za tathmini ya Mei, 2025 na mwelekeo wa Juni, 2025:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2025 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Juni, 2025 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Mei, 2025 vipindi vya mvua viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan yanayopata misimu miwili ya mvua, sambamba na vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo.


ii. Kwa mwezi Juni 2025, hali ya joto la chini inatarajiwa kupungua katika maeneo mengi ya nchi ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe (Juni-Agosti), 2025. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria, na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki na kusini magharibi.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2025.

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2025 baadhi ya maeneo nchini yaliendelea kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi, hususani maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Ongezeko la mvua lilijitokeza katika maeneo machache na kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji, uharibifu wa miundombinu na mali pamoja na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi. Aidha, kituo cha Zanzibar kiliripoti kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 101.0 kilichopimwa mnamo tarehe 01 Mei 2025. Ikifuatiwa na milimita 84.6 katika kituo cha Lyamungo mnamo tarehe 5 Mei na milimita 84.4 katika kituo cha Bukoba mnamo tarehe 13 Mei, 2025 . Vituo vingine vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Kwa upande mwingine, kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini ilisababisha vipindi vya upepo mkali uliofikia au kuzidi kasi ya kilomita 40 kwa saa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani na maziwa makuu.  Kwa upande wa hali ya joto, viwango vya joto la juu na la chini viliendelea kupungua katika baadhi ya maeneo. Kiwango cha juu zaidi cha joto cha nyuzi joto 32.7 °C kiliripotiwa katika kituo cha Dar es Salaam mnamo tarehe 22 Mei, na kiwango cha chini zaidi cha nyuzi joto 8.8 °C kiliripotiwa Igeri (Njombe) mnamo tarehe 24 na 26 Mei 2025.




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Mei, 2025

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2025

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2025, joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo kubwa la Bahari ya Hindi, huku eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la juu zaidi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani. Joto la Bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kati la kitropiki ya Bahari ya Pasifiki. Aidha. Hali ya joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) inatarajiwa kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu ya wastani katika ncha ya kusini mwa Afrika linatarajiwa kupunguza uwepo wa hewa yenye ubaridi kutoka kusini na hivyo kusababisha vipindi vichache vya baridi zaidi nyakati za usiku katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2025

Kipindi cha mwezi Juni 2025, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi hadi. Hata hivyo, hali ya baridi ya wastani hadi baridi kali inatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Singida pamoja na maeneo ya magharibi mwa mkoa wa Dodoma. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki na nyanda za juu kusini magharibi. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 25 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya nyuzi joto 14 °C na 22 °C katika maeneo ya nchi kavu. Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi **18** °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 16 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo yenye miinuko.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 18 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 katika kipindi cha mwezi Juni, 2025. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JULAI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hali ya ukavu na baridi inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kuendelea kujitokeza.

## 2.4 USHAURI

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Juni, 2025 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*